

Vingora za Moshi

Nyumbani

VINGORA ZA MOSHI NI MUHIMU

katika mpango wa kukwepa moto ya nyumbani.

Kukiwa na moto, moshi huenea haraka sana.

Vingora za moshi zinazofanya kazi zinakufahamisha mapema ili uondoke haraka.

VIDOKEZO VYA USALAMA

- Weka kingora za moshi katika kila chumba za malazi. Aidha, zinafaa kuwa nje ya kila chumba cha malazi na katika kila eneo nyumbani. Weka kingora katika gorofa ya chini.
- Vyumba vikubwa vinahitaji vingora zaidi za moshi.
- Ni vyema kutumia vingora zilizounganishwa. Kingora moja ya moshi iliapo, zote zinalia.
- Jaribu vingora zote za moshi angalau mara moja kwa mwezi. Bofya kitufe cha kujaribu kuhakikishakingora kinafanya kazi.
- Kengele za kisasa katika soko zinatumia teknolojia kadhaa zikiwemo kuhisi kwa haraka, ikiwemo mchanganyiko wa moshi na kabonmonoksaidi.
- Vingora za kisasa za moshi zina teknolojia ya kisasa ili kufahamu hali nyingi za moto, ili kuondoa kengele zenye hitilafu.
- Kingora cha moshi kinafaa kuwa juu ya dari ama juu zaidi katika ukuta. Weka vingora za moshi mbali na jikoni ili kupunguza vingora za kukosea. Zinafaa kuwa angalau futi 10 (mita 3) kutoka kwenye jiko.
- Watu wenye matatizo ya kusikia au viziwi wanaweza kutumia kengele maalum. Hizi vingora zina mwangaza mahsusi na vitingisha vitanda.
- Badilisha vingora za moshi zikiwa na miaka 10.



UKWELI

- ❶ Mlango uliofungwa unaweza kupunguza kuenea kwa moshi, joto, au moto.
- ❶ Vingora za moshi zinafaa kuwekwa katika kila chumba cha malazi, nje ya kila chumba cha malazi, na katika kila eneo. Vingora za moto zinafaa kuunganishwa ili moja ikilia, zote zinalia. Nyumba nyingi hazina ulinzi wa kiwango hiki.
- ❶ Takribani vifo 3 kati ya 5 hufanyika katika nyumba zisizo na Vingora za moshi ama vingora za moshi zisizofanya kazi.



**NATIONAL FIRE
PROTECTION ASSOCIATION**

The leading information and knowledge resource
on fire, electrical and related hazards